# OFISI YA MAKAMU WA RAIS
## WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

NA. 00000394 | TOLEO LA 42 - FEBRUARI 2022




## Toleo Maalumu

# SERA YA TAIFA YA MAZINGIRA YA MWAKA 2021 YAZINDULIWA


*Jarida hili limetolewa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini, S.L.P. 2502, Dodoma, Tanzania*

Ofisi ya Makamu wa Rais ofisi_ya_makamu_wa_rais @vpo_tanzania blog.vpo.go.tz

www.vpo.go.tz

# Yaliyomo



**Makamu wa Rais azindua Sera ya Taifa ya Mazingira, atoa maelekezo kwa viongozi** Uk. 3



**Dkt. Jafo: Mazingira ni agenda inayoimarisha uchumi** Uk. 10



**Dkt. Ndumbaro: Wananchi msikate miti ovyo** Uk. 12



**Wananchi watakiwa kufanya usafi kuepuka magonjwa ya mlipuko** Uk. 13



**Katibu Mkuu Maganga apongeza wananchi kushiriki Wiki ya Uzinduzi wa Sera ya Taifa ya Mazingira** Uk. 16

# Makamu wa Rais azindua Sera ya Taifa ya Mazingira, atoa maelekezo kwa viongozi




*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango akizungumza na viongozi, wadau wa mazingira, wanafunzi na wananchi mbalimbali juu ya uhifadhi wa mazingira wakati wa uzinduzi wa Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2021 uliofanyika katika viwanja vya Nyerere Square Jijini Dodoma.*

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Philip Mpango amezindua Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2021, uzinduzi uliofanyika katika viwanja vya Nyerere Square jijini Dodoma.

Makamu wa Rais alisema kazi ya kuhifadhi mazingira ikiwemo kulinda vyanzo vya maji, misitu,upandaji miti, kupendezesha miji, kufanya kusafi katika maeneo yote ya makazi na biashara, viwandani na masokoni ni lazima kuanzia sasa kuwa kazi za kudumu.

Aidha, alisema kuwa viongozi wote kuanzia ngazi ya vijiji hadi mikoa wanapaswa kusimamia uhifadhi wa mazingira na suala hilo litakuwa kipimo cha utekelezaji wa majukumu yao.

Dkt. Mpango alisema ni muhimu kuondoa nadharia katika uhifadhi wa mazingira ikiwemo kuwa na mipango isiotekelezwa bali inahitajika kazi ya ziada itakayotoa matokeo chanya katika kuhifadhi mazingira. Alisema sheria ndogondogo za uhifadhi wa mazingira zinapaswa kusimamiwa ikiwemo faini na ikiwezekana kuongeza faini hizo ili kukomesha waharibifu wa mazingira.

Alisisitiza kuwa zoezi la kutunza mazingira ni lazima kuwa shirikishi kwa wadau wote kuanzia mijini na vijijini na kuagiza wizara na taasisi zote za serikali kuhakikisha wanapanda miti na kuitunza katika maeneo yao.

Makamu wa Rais aliwataka Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) kutoa elimu kwa wananchi juu ya aina ya miti inayopaswa kupandwa kulingana na maeneo wanayoishi. Pia, aliwaasa kuhakikisha wanaongeza miche itakayopandwa ikiwemo kuongeza vitalu katika maeneo mbalimbali ili wananchi wapate urahisi wa kupata miche hiyo.

Makamu wa Rais alitoa wito kwa wamiliki wa viwanda nchini kuzingatia misingi ya uzalishaji endelevu pamoja na kutumia teknolojia rafiki kwa mazingira ili kupambana na uchafuzi wa mazingira.

Katika hatua nyingine Makamu wa Rais aliagiza Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Wizara ya Maji, Wizara ya Kilimo, Wizara ya Maliasili na Utalii pamoja na Wizara ya Mifugo na Uvuvi kuhakikisha zinashirikiana kushughulikia suala la




*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango akimkabidhi Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira Dkt. Selemani Jafo kitabu cha Mkakati pamoja na Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2021 kwaajili ya utekelezaji mara baada ya kuzindua Sera hiyo katika Viwanja vya Nyerere Square Jijini Dodoma tarehe 12 Februari 2022.*

uharibifu wa mazingira unaofanywa kwenye chanzo cha mto Ruaha katika Bonde la Ihefu kutokana na kuingizwa kwa makundi makubwa ya mifugo pamoja na kuelekezwa maji katika mashamba makubwa bila kurejeshwa mtoni.

Kwa upande wake Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Dkt. Selemani Jafo alisema Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2021 imezingatia masuala mbalimbali ikiwemo Mpango wa Taifa wa miaka mitano, Mpango Endelevu, pamoja na Mpango wa miaka 15 ulioanza mwaka 2011 hadi 2012.

Dkt. Jafo alisema Sera hiyo inatarajiwa kuokoa uharibifu wa mazingira katika nchi pamoja na kuongeza fursa za kiuchumi kwa mtu mmoja mmoja na taifa kwa jumla.

Alisema tayari wizara imefanya zoezi la utoaji elimu ya uhifadhi wa mazingira na kuongeza kwamba kwa muda wa siku tano tayari jumla ya miti laki moja na elfu arobaini na moja imepandwa katika jiji la Dodoma pekee huku lengo likiwa ni kupanda miti milioni 14.5 nchi nzima kwa kuwashirikisha wanafunzi nchi nzima.

Kwa upande wake Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais, Bi. Mary Maganga alisema maandalizi ya Sera ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 2021 yametokana na kuongezeka kwa changamoto mpya za uharibifu wa mazingira ikiwemo uchafuzi wa mazingira unaotokana na taka zitokanazo na vifaa vya umeme, matumizi ya kemikali yasioendelevu, mabadiliko ya tabia ya nchi pamoja na changamoto ya shughuli za uchimbaji wa mafuta, madini na gesi.

Naye Mwenyekiti Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji, Viwanda, Biashara na Mazingira Mhe. David Kihenzile alisema ni muhimu Serikali kuanza haraka mchakato wa kutungia sheria na kanuni sera hiyo ili ianze kutekelezwa kwa ufanisi.

Mhe. Kihenzile alisema kuwa suala la upandaji miti linapaswa kuwa na mkakati maalumu utakaorahisisha zoezi hilo.

# Makamu wa Rais aongoza zoezi la Upandaji Miti Dodoma



*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Philip Mpango akiongoza viongozi mbalimbali, wananchi na wanafunzi katika zoezi la kupanda miti eneo la barabara ya Chimwaga - St. Peter Claver mkoani Dodoma ikiwa ni utangulizi katika kuzindua Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2021.*



*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Philip Mpango akiwa na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa wakishuhudia zoezi la upandaji miti likifanywa na wanafunzi wa St. Peter Claver ikiwa ni utangulizi katika kuzindua Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2021.*



*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Philip Mpango akizungumza na washiriki wa zoezi la upandaji miti lililofanyika eneo la barabara ya Chimwaga - St. Peter Claver mkoani Dodoma ikiwa ni utangulizi katika kuzindua Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2021.*



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Dkt. Selemani Jafo akipanda mti katika eneo la barabara ya Chimwaga - St. Peter Claver mkoani Dodoma ikiwa ni utangulizi katika kuzindua Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2021.*

**KAZI** ya kuhifadhi mazingira ikiwemo kulinda vyanzo vya maji, misitu, upandaji miti, kupendezesha miji yetu na kufanya usafi katika maeneo ya makazi yetu, masoko, sehemu za biashara, viwandani na kwenye taasisi mbalimbali za serikali kama shule na taasisi zisizo za kiserikali ni lazima kuanzia sasa ziwe za kudumu!.



**Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango**
Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

**KUANZIA** sasa katika ziara zangu zote nitakazofanya, ajenda yangu ya kwanza katika Mkoa husika itakuwa ni ukijanishaji, upendezeshaji na usafi wa mazingira wa mahali hapo.

**KUMBUKENI** kuwa, ni agizo la Mwenyezi Mungu kutunza mazingira yetu kwa faida yetu na vizazi vijavyo. Kwa Wakristo someni Biblia Takatifu Kitabu cha Mwanzo Sura ya 2:15 na kwa Waislam someni Quran Tukufu Sura ya 80 aya ya 24-33 zinazozungumzia utunzaji wa mazingira.

**SHERIA** zetu ndogondogo kuhusiana na suala zima la hifadhi na usimamizi wa mazingira ziwekwe bayana na kusimamiwa ipasavyo ikiwa ni pamoja na faini na adhabu mbalimbali zitakazohusika. Na kama hizo faini ni ndogo sana basi tuongeze ili waharibifu wa mazingira wawajibike ipasavyo! Tuwe makini na wakali zaidi kwenye hili. Nitapenda pia kuona utaratibu wa kushindanisha Mikoa na Taasisi katika uhifadhi na usimamizi wa mazingira unaimarishwa.

**NAZIAGIZA** Wizara na taasisi zote za Serikali kuhakikisha zinapanda miti na kutunza mazingira katika maeneo yao yanayowazunguka. Zoezi hili lifanyike pia katika kila kaya; shule zote kuanzia msingi hadi vyuo vikuu; kwenye maeneo ya taasisi za dini kote nchini; kwenye maeneo yanayomilikiwa na taasisi binafsi kama vile vituo vya kuuza mafuta; na pia kwenye maeneo ya viwanda.

**SERA** ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 2021 imeweka malengo na matamko mahususi ya Kisera yatakayowezesha kukabiliana na changamoto za mazingira nchini kwa ufanisi mkubwa.

**SERA** hii imezingatia fursa za kiuchumi katika hifadhi na usimamizi wa mazingira nchini ambazo hazikutambuliwa na Sera ya awali kama vile, Urejelezaji wa taka ambao unapunguza gharama za udhibiti wa taka na kuongeza kipato; Utengenezaji wa bidhaa rafiki kwa mazingira kama Mifuko mbadala ya plastiki, Majiko banifu na Mkaa mbadala

**SERA** hii imezingatia fursa za kiuchumi katika hifadhi na usimamizi wa mazingira nchini ambazo hazikutambuliwa na Sera ya awali kama vile, Biashara ya hewa ukaa katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.



Mhe. Dkt. Selemani Jafo
Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira)

**SERA** hii imezingatia kuwepo kwa mipango mipya ya maendeleo ya kitaifa na kimataifa ikiwemo Mpango Elekezi wa Miaka Kumi na Tano (2011/12 - 2025/26); Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2021/22-2025/26); Malengo ya Maendeleo Endelevu (2030) na Makubaliano ya Paris kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi.

**KATIKA** shughuli za upandaji miti zilizofanyika katika Wiki ya Uzinduzi wa Sera katika Jiji la Dodoma jumla ya miti 3,100 imepandwa kwa lengo la kurejesha hali ya asili ya mazingira iliyoharibika kutokana na shughuli za kibinadamu; Kuwa na mazingira safi ili kuboresha afya ya jamii.

**SERA** ya Taifa ya Mazingira ya kwanza iliandaliwa mwaka 1997 ikilenga kutatua changamoto sita (6) za mazingira zilizoainishwa kuwa tishio kwa ustawi wa nchi wakati huo ambazo ni; uharibifu wa ardhi, kutopatikana kwa maji safi na salama kwa wakazi wa mijini na vijijini, uchafuzi wa mazingira, upotevu wa makazi ya viumbe-pori na bioanuai, uharibifu wa makazi ya viumbe waishio majini na uharibifu wa misitu.



**Bi. Mary Maganga**
Katibu Mkuu - Ofisi ya Makamu wa Rais

**UTEKELEZAJI** wa Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 1997 umeleta mafanikio katika dhana nzima ya kuhifadhi mazingira nchini na imewezesha kutungwa na kutekelezwa kwa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira (2004) na Kanuni zake 25.

**MAANDALIZI** ya Sera ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 2021, yametokana na ongezeko la changamoto mpya za uharibifu wa mazingira unaosababishwa na mabadiliko ya kiuchumi na kiteknolojia ikiwa ni pamoja na shughuli za uchimbaji wa mafuta, gesi, madini, Mabadiliko ya Tabianchi na Usimamizi wa matumizi salama ya bioteknolojia ya kisasa na Viumbe Vamizi.

**CHANGAMOTO** mpya za uharibifu wa mazingira unaosababishwa na mabadiliko ya kiuchumi na kiteknolojia ni pamoja na uchafuzi wa mazingira unaotokana na taka zinazozalishwa mijini; taka zitokanazo na matumizi ya vifaa vya umeme na kieletroniki na matumizi yasiyoendelevu ya kemikali.

# Matukio ya Uzinduzi wa Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2021



*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Philip Mpango akizindua Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2021. Kushoto kwa Makamu wa Rais ni Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira Mhe. Dkt. Selemani Jafo na kulia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji, Viwanda, Biashara na Mazingira, Mhe. David Kihenzile. Februari 12,2022.*

*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Mpango akizindua Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2021. Kushoto kwa Makamu wa Rais ni Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira Mhe. Dkt. Selemani Jafo na kulia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji, Viwanda, Biashara na Mazingira, Mhe. David Kihenzile.*



*Washiriki wakiwa katika uzinduzi wa Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2021 uliofanyika katika viwanja vya Nyerere Square Jijini Dodoma.*





*Sehemu ya wajumbe wa Kamati ya Kampeni Kabambe ya Hifadhi na Usafi wa Mazingira wakifuatilia matukio mbalimbali wakati wa katika uzinduzi wa Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2021 uliofanyika katika viwanja vya Nyerere Square Jijini Dodoma.*

# Dkt. Jafo: Mazingira ni ajenda inayoimarisha uchumi

Waziri wa nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mhe. Dkt. Selamani Jafo amesema mazingira ndiyo ajenda inayosababisha uchumi kuwa imara.

Alisema hayo wakati akizungumza na wanafunzi kutoka shule mbalimbali, viongozi na wananchi walioshiriki zoezi la upandaji miti katika eneo la Medeli jijini Dodoma Februari 7, 2022.

Dkt. Jafo alisema kuwa uchumi imara ni matokeo ya utunzaji mazingira kwa kuwa ni chanzo cha mvua ambazo zinasaidia kujaa kwa maji katika mabwawa ya kufua umeme ambao hutumika katika viwanda.

"Ndugu zangu tukikosa mvua tutakosa umeme na tukikosa umeme viwanda vitashindwa kufanya kazi na vikishindwa kufanya kazi watu watakosa ajira na watu wakikosa ajira uchumi utaporomoka kwa hiyo agenda ya mazingira ni inasababisha hata uchumi kuweza kuwa imara," alisema.

Zoezi hilo ni miongoni mwa shughuli zilizofanyika kuelekea uzinduzi wa Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2021 uliofanywa na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango Februari 12, 2022.

Pia, Waziri Dkt. Jafo alitumia nafasi hiyo kutoa rai kwa wananchi kutumia mvua zinazonyesha katika maeneo mbalimbali nchini kupanda miti ikue na kurejesha mazingira katika hali nzuri.

Aliwashukuru wadau mbalimbali waliojitokeza na kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais wakiwemo Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), Halmashauri ya Jiji la Dodoma,



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mhe. Dkt. Selemani Jafo akizungumza na wanafunzi kutoka shule mbalimbali na wananchi walioshiriki zoezi la upandaji miti katika eneo la wazi la Medeli jijini Dodoma.*



*Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) Abdallah Hassan Mitawi akipanda mti katika eneo la wazi Medeli jijini Dodoma.*

wanafunzi na wananchi kwa ujumla kushiriki katika zoezi hilo.

Aidha, waziri huyo alihamasisha wanafunzi hao kupeleka ujumbe kwa wazazi wao kushiriki katika zoezi la kupanda miti katika maeneo yao ili kuifanya Dodoma kuwa ya kijani.

Kwa upande wake Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais, Bi. Mary Maganga alisema katika zoezi hilo wameweza kupanda ya aina mbalimbali ikiwemo ya matunda na kivuli.

Bi. Maganga alisema kuwa zoezi hilo ni limekwenda vizuri na wamejitokeza kwa wingi kushiriki kupanda miti pamoja na kuwepo kwa changamoto ya kuwepo kwa mvua

Serikali imeamua kuwa na Wiki ya Uzinduzi wa Sera iliyoanza leo Februari 7, 2022 ambayo inaambatana na shughuli mbalimbali za hifadhi ya mazingira ikiwa ni sehemu ya masuala ya msingi yanayoelekezwa katika Sera mpya.

Ikumbukwe kwamba Sera ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 2021 imeongeza wigo wa masuala na changamoto za mazingira zinazopaswa kufanyiwa kazi katika kipindi husika ili kuleta maendeleo endelevu na imezingatia changamoto mpya za kimazingira zinazoendelea kujitokeza kutokana na mabadiliko ya mifumo ya kiuchumi, kijamii na kimazingira yanayoendelea duniani.

Dhumuni la kuwepo kwa shughuli hizo ni kurejesha hali ya asili ya mazingira iliyoharibika kutokana na shughuli za kibinadamu kwa kuwa na zoezi la upandaji miti, kuboresha afya ya jamii na elimu ya utenganishaji taka kwa ajili ya udhibiti wa taka ngumu na kuwezesha urejelezaji wa taka kwenye bidhaa na huduma mbalimbali.



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mhe. Dkt. Selemani Jafo akipanda mti na wanafunzi kutoka shule mbalimbali na wananchi walioshiriki zoezi hilo katika eneo la wazi la Medeli jijini Dodoma.*

# Dkt. Ndumbaro: Wananchi msikate miti ovyo




*Waziri wa Maliasili na Utalii Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro akizungumza na wadau mbalimbali mara baada ya kushiriki zoezi la upandaji miti katika eneo la Iyumbu jijini Dodoma Februari 9, 2022 ikiwa ni mojawapo ya shughuli za Wiki ya Uzinduzi wa Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2021, zoezi lililoratibiwa na Ofisi ya Makamu wa Rais.*

Waziri wa Maliasili na Utalii Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro ametoa rai kwa wananchi kufanya matumizi endelevu ya misitu badala ya kukata miti ovyo hali inayoweza kusababisha ukosefu wa mvua.

Dkt. Ndumbaro alitoa rai hiyo wakati akizungumza na wadau mbalimbali mara baada ya kushiriki zoezi la upandaji miti katika eneo la Iyumbu jijini Dodoma Februari 9, 2022 ikiwa ni mojawapo ya shughuli za Wiki ya Uzinduzi wa Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2021, zoezi lililoratibiwa na Ofisi ya Makamu wa Rais.

Alibainisha kuwa asilimia 54 ya eneo la nchi yetu ambayo ni sawa na hekta 400 ni misitu, hivyo kila mwananchi analo jukumu la kuitunza na kuendelea kupanda miti mingine ili iendelee Tanzania iendelee kuwa ya kijani kuleta faida.

"Ndugu zangu faida za misitu tunazijua, misitu ni mali kwasababu watu wanaishi Mafinga mkoani Iringa na maeneo mengine misitu ndio biashara yao n ahata kule nchini Norway misitu inachangia sana kwenye GDP," alisema.

Aidha, Waziri Dkt. Ndumbaro aliongeza kuwa kutokana na umuhimu wa misitu hiyo asilimia 3.5 ya Pato la Taifa (GDP) inachangiwa na sekta hiyo hapa nchini hivyo alisisitiza umuhimu wa kuilinda.



*Kamishna wa Uhifadhi wa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) Prof. Dos Santos Silayo akishiriki zoezi la upandaji miti katika eneo la Iyumbu jijini Dodoma.*

Hivyo, aliipongeza Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kuratibu Wiki ya Mazingira kuelekea kilele cha uzinduzi wa Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2021 na kushiriki zoezi la upandaji miti kwa kushirikiana na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) katika msimu huu wa mvua waliotoa miche ya miti mbalimbali ambayo imepandwa leo katika eneo la Greenpark, Iyumbu jijini Dodoma.

Alisema miti hiyo itasaidia kukabiliana na madhara yatokanayo na mabadiliko ya tabianchi ambayo yameendelea kushuhudiwa kutokana na mabadiliko yake kuja na athari hasi nyingi zikiwemo kuongezeka kwa joto duniani, kuongezeka kwa baridi, pamoja na kubadilika kwa misimu ya hali ya hewa.

Kwa upande wake, Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais, Bi. Mary Maganga alitoa wito kwa wananchi kupanda miti katika maeneo yao ili kuendelea kuifanya nchi kuwa ya kijani na mfano wa kuigwa.

Bi. Maganga alisema zoezi la upandaji ni kielelezo cha kutoa hamasa na kuhamasisha maeneo mengine nchi nzima kupata uelewa kuhusu dhana nzima ya kuifanya nchi nzima kuwa ya kijani nay a mfano kupitia kampeni ya Kijanisha Dodoma.

Pia aliwashukuru wadau waliojitokeza katika zoezi hilo na wadau mbalimbali wa mazingira hatua itakayoleta hamasa kwa wananchi ili waweze kufanya shughuli za upandaji miti na kuhifadhi mazingira kuwa sehemu ya maisha yao.

Nae Kamishna wa Uhifadhi kutoka Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), Pro. Dos. Santos Silayo alisema nchi yetu imejaliwa kuwa na misitu ya aina mbalimbali ikiwemo ya kupanda na kuota.

Prof. Silayo aliwataka wananchi kuwa na utamaduni wa kuitunza misitu iliyopo kwani ina mchango mkubwa katika sekta ya viwanda ambayo imekwa kwa kasi kubwa hapa nchini.

Aliongeza kwa kusema kuwa katika miaka mitatu sekta iliyopita tulishuhudia viwanda takriban 800 vikiwemo vya kati na vikubwa vikianzishwa sambamba na ukuaji wa teknolojia huku akitolea mfano wa nguzo za umeme zinazozalishwa hapa nchini kutokana na misitu.

Kamishna huyo alisema Ukuaji wa viwanda umekwenda kwa kasi kubwa na hata tunashuhudia viwanda vya mkaa mbadala ambavyo vyote vinaleta mchango mkubwa katika kuhifadhi mazingira.

# Wananchi watakiwa kufanya usafi kuepuka magonjwa ya mlipuko

Naibu Waziri wa Afya, Mhe. Dkt. Godwin Mollel ametoa wito kwa wananchi kushiriki kikamilifu katika usafi wa mazingira katika maeneo yao ili kuepuka na magonjwa yanayotokana na uchafu.

Alitoa wito huo Februari 10, 2022 wakati akizungumza na wafanyabiashara na wananchi katika soko la Mavunde lililopo Kata ya Chang'ombe jijini Dodoma wakati wa zoezi la usafi wa mazingira.

Dkt. Mollel alisema kuwa uchafu wa mazingira katika maeneo mbalimbali yakiwemo ya biashara na makazi yanasababisha magonjwa ya mlipuko ambayo endapo mwananchi ataugua atalazimika kutafuta matibabu na hivyo kuharibu bajeti ya familia na uchumi wao.

"Mkifanya mazingira yenu kuwa mazuri gharama ya kusafisha mazingira yenu ni kidogo kuliko gharama mtakazotumia kwenda kujitibu magonjwa yanayotokana na uchafu wa mazingira.

"Mojawapo ya vitu ambavyo vitatuongezea uhai ni kufanya usafi, uchafu unapunguza umri wa kuishi kwa sababu watu wengi wanakufa mapema kwa sababu wanaugua magongwa yatokanayo na uchafu hivyo ni muhimu sote tufanye usafi," alitahadharisha.

Aidha, Naibu Waziri huyo alisema ipo haja kwa Sheria ndogo za Jiji la Dodoma kuwabana wananchi katika usafi wa mazingira pamoja na upandaji wa miti kama wanavyofanya kwenye kuezeka mabati ya rangi katika nyumba zao.

Kwa upande wake, Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais, Bi. Mary Maganga alisema kuwa kampeni ya kupanda miti inakwenda sambamba na usafi wa mazingira nchi nzima.

Alisema zoezi la usafi lililofanyika leo ni mwendelezo wa shughuli zilizopangwakatika wiki ya uzinduzi wa Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2021 itakayozinduliwa Februari 12, 2022 na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dk.Philip isdor Mpango.

Pia Bi. Maganga aliwapongeza na kuwashukuru wadau mbalimbali wa mazingira walioshiriki na wanaoendelea kushiriki katika shughuli mbalimbali za mazingira zinazoendelea jijini Dodoma kuelekea uzinduzi huo.



*Naibu Waziri wa Afya Mhe. Dk. Godwin Mollel akishiriki zoezi la usafi wa mazingira katika Soko la Chang'ombe jijini Dodoma Februari 10, 2022 ikiwa ni sehemu ya shughuli zilizofanyika katika Wiki ya Uzinduzi wa Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2021.*




*Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais Bi. Mary Maganga akifanya usafi wa mazingira katika Soko la Chang'ombe jijini Dodoma Februari 10, 2021.*

# Yajue Masuala yaliyojumuishwa kwenye Sera ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 2021

**Udhibiti wa taka za kielektroniki**



**Usimamizi na matumizi ya kemikali**



**Udhibiti wa uchafuzi katika shughuli za utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi**



# Yajue Masuala yaliyojumuishwa kwenye Sera ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 2021

**Mabadiliko ya tabianchi**



**Usimamizi wa matumizi salama ya bioteknolojia ya kisasa**



**Udhibiti wa viumbe vamizi**



# Katibu Mkuu Maganga apongeza wananchi kushiriki Wiki ya Uzinduzi wa Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2021



*Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais Bi. Mary Maganga akipanda mti katika eneo la Tambukareli Dodoma Februari 11,2022, ikiwa ni wiki ya Uzinduzi wa Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2021, iliyozinduliwa Februari 12, 2022 jijini Dodoma na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dk. Philip Isdor Mpango.*



*Balozi wa Mazingira na Mbunge wa Pandani Mhe. Mariam Omary Saidi akipanda mti katika eneo la wazi la Tambukareli jijini Dodoma Februari 11, 2022.*

Wananchi wamehamasika na kujitokeza kwa wingi kushiriki shughuli mbalimbali za mazingira zilizopangwa kufanyika katika Wiki ya uzinduzi wa Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2021 jijini Dodoma.

Miongoni mwa shughuli hizo ni pamoja na kupanda miti na kufanya usafi katika maeneo mbalimbali yakiwemo Tambukareli, Iyumbu, Ilazo na Soko la Majengo jijini humo.

Hayo yalisemwa Februari 11 na Katibu Mkuu wa Ofisi ya Makamu wa Rais Bi. Mary Maganga wakati akiwaongoza wananchi walioshiriki zoezi la kupanda miti katika eneo la Tambukareli jijini Dodoma.

Kwa upande wake Balozi wa Mazingira na Mbunge wa Pandani, Mhe. Mariam Omary Saidi aliwataka wakazi wa Dodoma kuhakikisha wanaitunza miti na mazingira ili kuifanya Dodoma kuwa ya kijani.

Awali, Kamishna Msaidizi wa Uhifadhi Wakala wa Huduma za Misitu (TFS), Kanda ya Kati, Mathew Kiondo alihimiza wananchi waitunze miti hiyo baada ya msimu wa mvua kuisha na kudhibiti mifugo.

Alisema si busara kupanda miti leo halafu mwakani tena tunapanda sehemu ile ile, hii ni kupoteza nguvu na fedha za Serikali hivyo alihimiza kuhakikisha miti inapandwa leo.

Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2021 ilizinduliwa na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dk.Philip Isdor Mpango jijini Dodoma Februari 12, 2022.

# Matukio mbalimbali ya Wiki ya Uzinduzi wa Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2021



*Naibu Waziri wa Afya Mhe. Dk. Godwin Mollel (mwenye Kaunda suti) na Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais Bi. Mary Maganga wakipita katika maeneo mbalimbali ya soko la Chang'ombe jijini Dodoma Februari 10, 2022 kuhamasisha usafi wa mazingira ikiwa ni sehemu ya shughuli zilizofanyika katika Wiki ya Uzinduzi wa Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2021.*



*Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) Bw. Edward Nyamanga akikusanya taka katika kizimba cha Soko la Chang'ombe jijini Dodoma wakati wa zoezi la usafi wa mazingira sokoni hapo Februari 10, 2021.*



*Wananchi wakishiriki katika zoezi la usafi wa mazingira katika cha Soko la Chang'ombe jijini Dodoma wakati wa zoezi la usafi wa mazingira sokoni hapo Februari 10, 2021.*



*Wananchi wakishiriki katika zoezi la usafi wa mazingira katika eneo la Ilazo jijini Dodoma Februari 8, 2022 ikiwa ni miongoni mwa shughuli zilizofanyika katika Wiki ya Uzinduzi wa Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2022.*

# Matukio mbalimbali ya Wiki ya Uzinduzi wa Sera ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 2021




*Mkurugenzi wa Mazingira Ofisi ya Makamu wa Rais Dk. Andrew Komba akishiriki ozei la usafi wa mazingira katika Soko la Chang'ombe jijini Dodoma Februari 10, 2022 katika Wiki ya uzinduzi wa Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2021.*



*Mkurugenzi Msaidizi wa Idara Mazingira Ofisi ya Makamu wa Rais Bw. Faraja Ngerageza akitoa elimu kwa wanafunzi kuhusu upandaji miti na mazingira kwa ujumla kabla ya zoezi la upandaji miti katika eneo la wazi la Medeli jijini Dodoma Februari 7, 2022.*



*Mwanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Medeli akipanda mti wakati wa zoezi la upanda miti katika eneo la wazi la Medeli jijini Dodoma Februari 7, 2022.*



*Wanakikundi cha usafi wa mazingira wakikikusanya na kupakia taka katika gari kwa ajili la kwenda kumwagwa kwenye dampo wakati wa zoezi la usafi wa mazingira uliofanyika katika eneo la Ilazo jijini Dodoma Februari 8, 2022.*









**Limetolewa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini**
**Ofisi ya Makamu wa Rais**
S.L.P. 2502, Dodoma, Tanzania
Simu: +255 266 235 2038 • Nukushi +266 235 0002
Barua pepe: km@vpo.go.tz • Tovuti: www.vpo.go.tz
Simu ya mkononi: 0685 333 444
Facebook: Ofisi ya Makamu wa Rais
Instagram: ofisi_ya_makamu_wa_rais
Twitter: @vpo_tanzania
Blog: blog.vpo.go.tz